**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**


**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA,**
S. L. P 92,
CHATO.


**Tarehe: …………**


***MKUU WA SHULE: 0754068201/O628568201***

***MAKAMU MKUU*: *WA SHULE: 0782909776***

Iparamasasecondary2007@gmail.com


Kumb.Na.ISS/ADM/F.V/*2026/2027*

**MZAZI/MLEZI WA ______________________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA MWAKA ……… MCHEPUO WA: HGL NA HKL.**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Iparamasa mwaka …………... **HONGERA SANA NA KARIBU SANA.**

**1. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Iparamasa ipo mkoa wa Geita wilaya ya Chato umbali wa kilometa ishirini (20) kutoka mji wa Buseresere/Katoro. Shule ipo jirani na kituo cha afya cha Iparamasa.

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA IPARAMASA SEKONDARI.**

Kwa wanafunzi wanaotoka mkoa wa Kigoma, Kagera na ukanda wa kahama wapande magari ya kwenda Geita au Mwanza, wateremkie Katoro. Baada ya hapo wapande pikipiki za kwenda Iparamasa kiasi cha shilingi elfu nne (4,000/=) mpaka shuleni.

Kwa wanaotoka mikoa ya Mara, Shinyanga, Arusha, Simiyu, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Dar es salaam, wapande magari yanayokwenda Mwanza. Wakifika Mwanza wapande magari yaendayo Katoro au magari yaendayo mojawapo ya wilaya za Chato, Bukombe, Biharamulo na Bukoba wateremkie Katoro. Baada ya hapo wapande pikipiki za kwenda Iparamasa kiasi cha shilingi elfu nne (4,000/=) mpaka shuleni

*Kiambatisho (b)*

**SHERIA ZA SHULE**
Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.


Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii, utatakiwa kushika na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujua sheria hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

**SARE YA SHULE**
Wakati wote wa muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni suruali ya Dark Blue na shati nyeupe (mikono mirefu). Baada ya muda wa masomo, siku za sikukuu pamoja na Jumamosi na Jumapili sare ni suruali ya Kaki na T-sheti ya shule. Tracksuit itavaliwa muda wa michezo na usafi wa mazingira. **Kwa sababu yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuvaa nguo za kiraia (asije nazo kabisa).**

Pamoja na barua hii naambatisha viambatisho vifuatavyo.
(a) Orodha ya mahitaji,
(b) Mchanganuo wa malipo.
(c) Sheria za shule
(d) Fomu ya kukubali
(e) Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi,
(f) Fomu ya mzazi/mlezi
(g) Fomu ya hospitali.

**4.KUFUNGUA SHULE**
Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **……………….**

**ANGALIZO; Shule haipokei fedha taslimu kiwango chochote. Malipo yote yafanyike tawi lolote la benki ya NMB au Wakala wa NMB kupitia akaunti za shule zilizotolewa katika kiambatisho (b).**




YALED ISAYA YANDOKOLA
**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA**

## MAHITAJI (a) Vifaa

- Suruali mbili Dark Blue za kushona **zisizobana mwili (modal)** zenye malinda 4 na ‘turn up’
- Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
- Tai ya Dark Blue
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu wala shingo ndefu.
- Mkanda mweusi wa suruali usio na chuma kikubwa wala maandishi.
- Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
- Sweta rangi ya kijivu cheusi (Charcoal Grey)
- T-shirt moja ya kijivu yenye nembo ya shule inapatikana shuleni Tsh 12,000/=
- Godoro imara la super banco, QFL Dodoma au Best Arusha futi 2 ½ kwa futi 6
- Shuka ‘pair’ 2 rangi ya bluu kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- Chandarua ya rangi nyeupe na foronya/mto rangi ya bluu.
- Ndoo mbili lita 10 kwa ajili ya kuchotea maji ya kuoga na matumizi mengine.
- Sahani, bakuli, kikombe, bna kijiko kwa ajili ya chakula.
- Kandambili kwa ajili ya kuogea **tu**.
- Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
- Track suit rangi ya Dark Blue
- Ufagio wa plastiki wa dukani (soft bloom), raba (mopper) kwa ajili ya kudekia, jembe lenye mpini, na kwanja (fyekeo),
- Ream ya karatasi nyeupe A4 (kila muhula) kwa ajili ya mazoezi ya darasani
- Shajala moja (file za plastic) na picha –passport size 2 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa/uraia (siyo kadi ya kliniki).
- Hati maalum ya vipimo kutoka kwa daktari kuthibitisha afya yako.
- Nakala ya taarifa ya matokeo kidato iv (result slip)
- **Advanced Learner’s Dictionary** (ni lazima.)
- Madaftari makubwa saba (counter book 4 Quires) na madaftari madogo saba
- Kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa
- Sanduku/Trunker la kutunzia mali zake.

## (b) Malipo

- ✓ Mchango wa Uendeshaji Wa Shule Tsh. 65,000/=
- ✓ Tahadhari Tsh. 5,000/=
- ✓ Nembo Tsh. 5,000/=
- ✓ Kitambulisho cha Shule Tsh. 5,000/= **JUMLA. Tsh. 80,000/=**

***( C ) Bima ya Afya.***

Jukumu la matibabu ni la mzazi, hivyo mzazi/mlezi anashauriwa kumlipia mtoto wake bima ya afya ya Taifa (NHIF) ambapo shule itawaunganisha na ofisi za NHIF mkoa wa Geita kupata bima hizo. ***Kila mwanafunzi ni lazima aje na bima ya afya ya NHIF. Kwa wale wasiokuwanazo waje na shilingi 50,400/=*** ili wapatiwe bima hizo na ofisi za bima (NHIF) ya mkoa wa Geita. Malipo hayo ya bima ni kwa mwaka.

**MCHANGANUO WA MALIPO NA VIFAA**

**1.** Michango **YOTE** iwekwe katika akaunti ya shule inayoitwa "IPARAMASA SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT" Na. **32701200068 NMB:**

| **Na.** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | Tsh. 65,000/= |
| 2. | Nembo ya shule | Tsh. 5,000/= |
| 3. | Tahadhari | Tsh. 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | Tsh. 5,000/= |
| | **JUMLA** | **Tsh. 80,000/=** |

**2. Vifaa vya kuleta shuleni ni hivi vifuatavyo**:
Mzazi/mlezi unasisitizwa kukamilisha michango kwa wakati ili kuepuka usumbufu. Kwa ufafanuzi endapo utapata utata piga Na ***0754068201/O628568201/0782909776.***

| **NA** | **AINA YA KIFAA** | **IDADI** |
|---|---|---|
| 1. | Ream ya karatasi A4 2 kwa Mwaka | 02 |
| 2. | Ufagio wa dukani au reki | 01 |
| 3. | Jembe na Mpini wake | 01- HGL |
| 4. | Kwanja (fyekeo) | 01- HKL |
| 5. | Ndoo ndogo lita 10 | 02 |
| 6. | Shajala (file la plascic) | 01 |
| 7. | Raba (Mopper) kwa ajili ya kudekia | 01 |
| 8. | Kidumu cha lita 5 | 01 |
| 9. | Sabuni ya maji kwa ajili ya usafi wa vyooni | Lita 5 |

*Kiambatisho ( c )*

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO
**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA**

**SHERIA ZA SHULE**

**(a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE**

1.**HESHIMA**:

Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.

2**. MAWASILIANO**:

Kingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni,hivyo mwanafunzi haruhusuwi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midaharo ya Kiswahili.

3.**USAFI**: Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

4.**RATIBA YA SHULE**:

Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii wito (**kengere.)**

**(b) MAKOSA YA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI**.

1. Wizi wa aina yoyote.
2.Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Ulevi wa pombe/madawa ya kulevya kama vile mirungi,kuber,bangi n.k
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/jamii
5.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6.Kudharau bendera ya Taifa
7. Kuoa/kumpa mimba msichana
8.Kugoma, kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni /jamii
9.**Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi**
10.Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani
11.Kugomea adhabu yoyote halali
12. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule na bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule
13.Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe
14.Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa

*Kiambatisho (e)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA**

**ANGALIZO Na.1:** ***Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa na simu atatozwa faini ya kununua umeme wa shule wa shilingi laki mbili (Tsh. 200,000/=) Hivyo mzazi hakikisha mwanao hamiliki simu kwa namna yoyote ile ili kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima*. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

**(c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1.Utoro wa aina yoyote.
2.Kuchelewa kufika shuleni (baada ya likizo) na katika shughuli mbalimbali za shule.
3. Kutokuvaa sare rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule
4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele,kutokuoga n.k ) na kutokutunza mazingira ya shule
5. Kuonekana nje ya mipaka ya shule bila kibali

6. **ANGALIZO Na.2:** ***Mwanafunzi atakayebainika*** **kuonekana nje ya mipaka ya shule bila kibali,** ***atatozwa faini ya kuleta tofali za block 20 au mfuko mmoja wa simenti. Hivyo mzazi zungumza na mwanao atulie shuleni au kufuata taratibu za kutoka nje ya shule Ili kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima*.**

**TANBIHI**: Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi, heater,n.k. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kumiliki redio yenye kubeba memory card/frash**. Kwa kuwa mwanafunzi haruhusiwi kumiliki line/simu, shule itaweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu ya mkuu wa shule na waandamizi wake *0754068201/ O628568201/ 0782909776***

*Kiambatisho (e)*

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**
**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA**

**SHULE YA SEKONDARI IPARAMASA,**
**S.L.P 92,**
**CHATO.**
**TAREHE: ………..**

**KUMB.NA.ISS/ADM/FV/…..**

**FOMU YA KUKUBALI**

Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi) ____________________________

Mimi…………………………………… (mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha …………….katika shule ya sekondari Iparamasa. Pia nimesoma na kuelewa maelekezo yote yaliyomo katika fomu hii,naahidi kuyazingatia **yote** ikiwa ni pamoja na kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika migomo na maanadamano yasiyoruhusiwa.

| | |
|---|---|
| ………………………<br>Saini ya mwanafunzi | …………….<br>tarehe |

Mimi…………………………………………….. mzazi /milezi wa …………….. (mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote yaliyomo katika fomu ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari Iparamasa na ninakubali na kuahidi kwamba nitawajibika sawasawa kwa jambo lolote linalomhusu mwanagu. Aidha nitakuwa tayari kushirikiana na walimu kuhakikisha mwanangu anamaliza elimu ya kidato cha sita kwa kuwajibika kulipa michango ya shule pamoja na maelekezo megine yatakayokuwa yakitolewa na shule.

| | |
|---|---|
| …………………………..<br>Saini ya mzazi/Mlezi | …………………<br>tarehe |

*Kiambatisho (f )*

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

1. Jina kamili …………………………………………… …….
2.(a)Tarehe ya kuzaliwa …………………………………… …
(b)Mahali alipozaliwa……………………………………… …
3.(a) Dini……………………… …………………………..
(b) Dhehebu…………………………………………………
4.(a) Uraia…………………………………………………. ….
(b) Kama siyo raia wa Tanzania taja uraia wako ……………
5. Shule ya sekondari uliyotoka…………………………………
6. (a) Jina kamili la mzazi /mlezi………………………………
(b) Anwani ya mzazi/mlezi…………………………………
(c) Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………
(d)Kituo chake cha kazi………………………………………
(e)Namba ya simu……………………………………………
7. (a) Mahali anapoishi……………………………………………
(b) Jina la mwenyekiti wa kitongoji/mtaa ……………………
8. (a) Je, unaishi na nani?
Taja jina kamili …………………………………………………
(b) Je,una uhusihano gani na huyu uliyemtaja?............................
9.Ni yatima/si yatima…………………………………………….
10.Kama ni yatima mzazi yupi aliyefariki? Mama/baba/wote ……


***Attachment (g)***

IPARAMASA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 92,
CHATO.
Date: …………..

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
MEDICAL OFFICER IN CHARGE
………………………………………
…………………………………...…

STUDENT'S NAME..................................................................…

Please examine the above named student as to his physical/mental fitness/unfitness for admission as full time student of Iparamasa Secondary School for academic year 2026/2027.
The examination should include the following categories: Eye sight, Hearing, Epilepsy, Urine,
Venereal disease, Stool and any other
body deformation




YALED ISAYA YANDOKOLA
MKUU WA SHULE

THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE
-----------------------------------------------
-----------------------------------------------
-----------------------------------------------

THE HEADMASTER,
IPARAMASA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 92,
**CHATO.**

**RE: MEDICAL EXAMINATION RESULTS**

I have examined the above student and found him with the following disease/ impairment/disabilities:

Eye sight…………………………………………………………………
Urine examination……………………………………………
Hearing …………………………………………………
Stool examination………………………………………………………
Speech ………………………………………………………………………
Venereal diseases…………………………………………………………
Limbs…………………………………………………………………
Epilepsy………………………………………………………………
Additional information/other serious diseases……………………………………..
……………………………………………………………

**Medical remarks**

…………………………………………….  …………..………………………
…………………………………… ………..………………………………………
….…………………………………………………………………………………
…………..  ……………………………………………………………………..
……………………………………..  ……………………………………………..
…………………………… ……………………………………………………….

Name and signature of attending officer…………..…………Date……………

Designation………………………………. Official stamp……………………